BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Sita – Tarehe 20 Septemba, 2023
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kwa mwaka 2022/2023.

### Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kwa mwaka 2022/2023.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii Kuhusu Ripoti ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda juu ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Ripoti ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kwa mwaka 2022/2023.

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii Kuhusu Ripoti ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo juu ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Ripoti ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kwa mwaka 2022/2023.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

65. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Tunaipongeza Serikali kwa kutuwekea vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi ambavyo vina umuhimu mkubwa na vinatumika katika masuala mbali mbali ya kimaendeleo. Hata hivyo, kuna changamoto mbali mbali zinazoambatana na vitambulisho hivyo.

Kwa nini kwenye kitambulisho Karani anapokosea kuandika jina adhabu ya kutozwa Tsh. 42,000/- anapewa mwenye jina ili jina lake liandikwe vizuri.

### Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

51. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kiwanja cha Magirisi ni miongoni mwa viwanja vinavyotumika kwa shughuli mbali mbali za kijamii na kisirekali.

Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kukifanyia ukarabati kiwanja hiki, ili kikidhi haja ya mahitaji hayo.

59. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

(a) Kwa sasa Waandishi wa Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) wanapokuja kuchukua taarifa za nje ya eneo la kazi wanatakiwa kulipwa posho la kiasi gani kwa kila mmoja.

(b) Je, utaratibu huu wa kuwalipa posho zao nje ya maeneo yao ya kazi unafuatwa ipasavyo na taasisi nyengine za binafsi na Serikali.

### Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

12. MHESHIMIWA MTUMWA PEYA YUSSUF (Jimbo la Bumbwini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Katika ujenzi wa skuli za ghorofa kupitia fedha za UVIKO 19 (COVID 19), imebainika kuwa ujenzi wa baadhi ya skuli hizo haukuzingatia miundombinu rafiki kwa Watu Wenye Ulemavu, kwa maana ya kutowekwa kwa “lift” au ngazi za mzunguko.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawekea miundombinu rafiki Watu Wenye Ulemavu kupitia ujenzi wa skuli hizo.

(b) Kwa nini katika matayarisho ya ujenzi wa skuli hizo, haikushirikishwa Idara ya Watu Wenye Ulemavu.

## Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

32. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Je, ni kwa kiasi gani uwepo wa bandari bubu na Mabadiliko ya Tabia Nchi unachangia uvamizi wa wadudu waharibifu wa mazao ya kilimo kutoka maeneo ya nje ya nchi yetu

## Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

82. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya kutatua au kutafuta ufumbuzi wa changamoto ya maji safi na salama katika sehemu tofauti, bado kuna maeneo ambayo hayapati maji safi na salama, ikiwa ni pamoja na eneo la Chukwani upande wa Baraza la Wawakilishi, upande wa Msikiti Mwekundu, Sumai, kwa Mahita, upande wa Coconut na maeneo mengine ya Chukwani.

(a) Je, kwa kiasi gani Serikali inalifahamu tatizo hilo.

(b) Ni upi mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kuwa huduma hiyo inapatikana ipasavyo katika maeneo ya Chukwani.

**Wizara ya Afya:**

15. MHESHIMIWA MTUMWA PEYA YUSSUF (Jimbo la Bumbwini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

    Baadhi ya wafanyakazi wa Idara ya NED ya Wizara ya Afya wanadai malimbikizo ya madeni ya kambi tokea mwaka 2019 hadi sasa.

    (a) Je, ni lini watalipwa madeni hayo.

    (b) Kwa kuwa kazi zao ni ngumu, Je, Wizara yako haioni kuwa kutowalipa madeni yao kunawapunguzia nguvu ya kufanya kazi wafanyakazi hao.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

27. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

    Je, ni maeneo gani ambayo wataalamu wa Mambokale wameshiriki au kushirikishwa katika kufanya "Heritage Assessment" kutokana na ukarabati wa ujenzi unaoendelea katika maeneo mbali mbali ndani ya mji wa Zanzibar kwa hivi sasa.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

Ripoti ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kwa mwaka 2022/2023.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

Ripoti ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kwa mwaka 2022/2023.

Zanzibar,
20 Septemba, 2023.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.